# هَدْيُ الإِمَامِ الرِّضَا فِي صَلَاةِ الجَنَازَةِ

## (الدُّعَاءُ عَلَى السُّنِّيِّ بِاللَّعْنِ وَالخِزْيِ وَالعَذَابِ الأَلِيْمِ)

# MWONGOZO WA IMAM RIDHWA KATIKA SWALA YA JENEZA

## (kumuombea Sunni laana, udhalili na adhabu kali)

Amesema Imam Ridhwa (mmoja wa maimamu wa Kishia):

"وَإِذَا كَانَ المَيِّتُ مُخالِفًا فَقُلْ فِيْ تَكْبِيْرِكَ الرَّابِعَةِ: "اللَّهُمَّ اخْزِ عَبْدَكَ وَابْنَ عَبْدِكَ هَذَا، اللَّهُمَّ اصْلِهِ نَارَكَ، اللَّهُمَّ أَذِقْهُ عَلِيْمَ عِقَابِكَ وَشَدِيْدَ عُقُوْبَتِكَ، وَأَوْرِدْهُ نَارًا وَامْلَأْ جَوْفَهُ نَارًا، وَضَيِّقْ عَلَيْهِ لَحْدَهُ، فَإِنَّهُ كَانَ عَادِيًا لِأَوْلِيَائِكَ وَمُوَالِيًا لِأَعْدَائِكَ، اللَّهُمَّ لَا تُخَفِّفْ عَنْهُ الْعَذَابَ وَاصْبُبْ عَلَيْهِ العَذَابَ صَبًّا. فَإِذَا رُفِعَ جَنَازَتُهُ فَقُلْ: اللَّهُمَّ لَا تَرْفَعْهُ وَلَا تُزَكِّهِ"

**"Ikiwa maiti ni Mukhaalif (si katika Mashia), sema katika Takbira yako ya nne: [Ewe Allaah mdhalilishe mja wako huyu na mtoto wa mja wako. Ewe Allaah muingize katika moto wako. Ewe Allaah muonjeshe yeye uchungu wa adhabu yako na ukali wa mateso yako. Na muingize katika moto wako na ujaze kaburi lake moto, na ufanye finyu juu yake mwanandani wake, kwa sababu alikuwa ni adui wa vipenzi vyako na kipenzi wa maadui zako. Ewe Allaah usimpunguzie yeye adhabu yako na umimine juu yake adhabu nyingi]. Na likinyanyuliwa jeneza lake utasema: [Ewe Allaah usimpandishe yeye daraja wala usimtakase][1].**

**Ndugu Muislamu,** hii ndio dua ambayo Shia humuombea kila maiti asiyekuwa Shia, kwa hiyo usidhani kwamba Mashia wanahudhuria katika jeneza la Sunni ni kwa ajili ya kumuombea pepo na kuepushwa na moto Hapana! Wanahudhuria ili kumuombea laana na adhabu!.

---

[1]- Tazama kitabu: [Al Fiqhi] (Uk. 178). Kitabu hiki kinanasibishwa na Imamu wa nane wa Kishia Abul Hasan Ally Bin Musa (Imam Ridhwa), amezaliwa mwaka 148H-766M na amefariki 202H-818M.

**Maana ya neno Mukhaalif na 'Aammah mbele ya Maulamaa wa Kishia:** Amesema mwanachouni wao mkubwa (Ayatolah) Muhammad Said Al Hakim katika kitabu chake [Al Muhkam Fiy Usuulil Fiqh] (Jz. 7, Uk. 182), wakati akifafanua maana ya neno Al Mukhalif na Al 'Aammah:

"الظَّاهِرُ أَنَّ الْمُرَادَ بِالْعَامَّةِ الْمُخَالِفُوْنَ الَّذِيْنَ يَتَوَلَّوْنَ الشَّيْخَيْنِ وَيَرَوْنَ شَرْعِيَّةَ خِلَافَتِهِمَا"

**[Dahiri ni kwamba makusudio ya neno Al 'Aamah ni Mukhaalifun[2] ambao wanawapenda masheikh wawili (Abubakar na Omar), na waona kwamba Ukhalifa wao ni wa-kisheria][3].**

Pia Zainud Diyn Al 'Aamiliy katika kitabu chake: [Ar Raudhatul Bahiyyah] (Jz. 1, Uk. 428), wakati akielezea kwamba Takbira katika swala ya maiti ni tano isipokuwa kwa Mukhaalif, akasema katika ta'liq:

"لِأَنَّهُ يَجِبُ الِاقْتِصَارُ عَلَى الرَّابِعِ تَكْبِيْرَاتٍ فِي الصَّلَاةِ عَلَى الْمُخَالِفِ وَهُوَ غَيْرُ الإِثْنَيْ عَشَرِيِّ مِنْ فِرَقِ الْمُسْلِمِيْنَ"

**"Hakika ni wajibu kukomea takbira ya nne katika kumswalia Mukhaalif, naye ni kila muislamu asiyekuwa Shia Ithnaasharia".**

Pia haifai kwa Shia kuosha maiti ya asiyekuwa Shia isipokuwa kwa dharura, kama alivyosema hayo mwanachuoni wao mkubwa Muhammad Bin Nu'man Al-Mufid kwenye kitabu chake: [Al Muqni'a] (Jz. 1, Uk. 144):

"وَلَا يَجُوْزُ لِأَحَدٍ مِنْ أَهْلِ الإِيْمَانِ أَنْ يَغْسِلَ مُخَالِفًا لِلْحَقِّ فِي الْوَلَاءِ وَلَا يُصَلِّيَ عَلَيْهِ إِلَّا أَنْ تَدْعُوَهُ ضَرُوْرَةٌ إِلَى ذَلِكَ مِنْ جِهَةِ التَّقِيَّةِ فَيَغْسِلُهُ تَغْسِيْلَ أَهْلِ الْخِلَافِ وَلَا يَتْرُكُ مَعَهُ جَرِيْدَةً وَإِذَا صَلَّى عَلَيْهِ لَعَنَهُ فِيْ صَلَاتِهِ وَلَمْ يَدْعُ لَهُ فِيْهَا"

**"Wala haifai kwa yeyote katika watu wa Imani[4] (Mashia) kumuosha wala kumswalia Mukhaalif (mwenye kupinga) haki ya Ukhalifa (wa Ally Allaah amridhie), isipokuwa ikimpelekea yeye dharura ya kufanya hivyo, katika kuifanyia kazi taqiyyah[5], hapo**

---

2- Maana ya Mukhaalif ni mpingaji na 'Aammah ni mtu wa kawaida asiye na elimu (mjinga).

3- Masheikh wawili hapo ni Abubakar na Omar -Allaah awaridhie- kama alivyotaja hilo Al Majlis.

4- Anasema Khomein: "Ahlul Imani (watu wa Imani ni: **Shia Imaamiyyah Al Ithnaasharia"**. Angalia: [Al Makaasibul muhaaramah] (Jz. 1, Uk. 378).

5- Taqiyyah maana yake ni: **"Kuficha Itikadi ya Shia mbele ya asiyekuwa Shia, na kuyaeneza madhehebu hayo kwa siri**. Amesema haya sheikh wao Muhammad Swadiq Ar Ruuhaniy katika kitabu chake: [Fiqhu Swadiq] (Jz. 11, Uk. 418).

**atamuosha josho la watu wapinzani, na wala asimuache na nguo, na ikimswalia atamlaani katika swala yake wala asimuombea dua ya kheri katika swala hiyo".**

Ewe ndugu yangu Muislamu, je, umeona mafunzo ya dini ya Shia katika kumswalia maiti asiyekuwa Shia?, hakuna kumuombea kheri isipokuwa ni laana tu! Je, huu ndio udugu ambao wanaudai katika maneno yao!

## Mambo ya kutafakari kwenye mwongozo huu wa Mashia:

1. Je, kwa maneno hayo yaliyotangulia kutoka kwa Maulamaa wa Kishia, vipi itawezekana Shia na Sunni kuungana pamoja?
2. Je, Dua hii ndio ya kumuombea ndugu yako Muislamu wakati wa ukimswalia, au Shia hamzingatii Sunni kuwa ni Muislamu?
3. Je, hii si ishara ya kuwakufurisha Waislamu pasi na hoja za msingi?
4. Je, ikiwa hali ndio hii, itafaa kwa Sunni kumtanguliza Shia kuswalia jeneza la ndugu yake?
5. Je, mafunzo haya yapo ndani ya Qur'an au Sunnah, au Mashia wana mwongozo mwingine usiokuwa viwili hivyo?

Allaah ndiye mwenye kuongoza kwenye njia ya sawa.

**Ameandika:**
**Abu Halima Arafat Ibn Mahmoud**
**Usiku wa jumapili tarehe 1/Muharram/1446h – 7/7/2024m**
**Pongwe -Tanga**